

3SquaresVT

Mpango wa Vermont wa Usaidizi wa Lishe ya Ziada
[Vermont's Supplemental Nutrition Assistance Program (ilikuwa ikiitwa Food Stamps)]

Kwa Wahamiaji

Nani anastahili?

Unaweza kufanya maombi ya usaidizi wa chakula wa 3SquaresVT, bila kujali tarehe uliwasili Marekani, kama wewe:

- ◆ una umri wa chini ya miaka 18
- ◆ umepata hifadhi au ni mkimbizi
- ◆ unapokea marupurupu ya ulemavu
- ◆ mhamiaji kutoka Cuba au Haiti
- ◆ mtu uliyeruhusiwa kubaki nchini badala ya kuondoshwa
- ◆ ni wa asili ya Amerasia
- ◆ ni wa kabila la Hmong au Highland Lao
- ◆ ni Mwamerika Asilia (American Indian) aliyezaliwa Canada
- ◆ ni mtu mwenye uhusiano na jeshi la Marekani
- ◆ ni mdhulumiwa wa uhasama wa nyumbani (domestic violence)

Kama wewe ni **Mkaazi Halali wa Kudumu (Legal Permanent Resident)** asiyetimiza lolote kati ya masharti haya hapa juu, unaweza kupata marupurupu tu kama **umeishi Marekani kwa miaka mitano** au una **“robo zinazostahili” 40** (mda wa miezi 3) **ya kazi**. Robo zinaweza kupatikana na mwenye kufanya maombi, wazazi wake na/au mume/mke wake.

Wahamiaji wote ni sharti wawe wanaishi Marekani kihalali na watimize mahitaji ya mapato, malimbikizo na wengineo ndipo waweze kustahili kupata marupurupu ya 3SquaresVT. Kwa maelezo zaidi au uweze kupata fomu ya maombi:

1-800-479-6151

www.vermontfoodhelp.com



*Ujumbe huu umedhaminiwa kwa kiasi na USDA,
Mpena nafasi tena muajiri kwa usawa.*

4/10/09

